JINA……..……NAMBA YAKO……..

SHULE……..…….. SAHIHI ……..……

TAREHE……..

102/2
KISWAHILI
Karatasi la Pili
LUGHA
Saa: 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI-MUUNGO WA SHULE ZA UPILI ZA AINAMOI NA BELGUT 2010

MAAGIZO

- *Andika jina lako na mambari yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.*
- *Weka sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoaciwa hapo juu.*
- *Jibu maswali yote*
- *Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu cha maswali.*
- *Karatasi hii ina kurasa 12 zilizopigwa chapa.*
- *Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU:

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	Jumla	

1. UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Ulimwengu unapaswa kuzuka na mbinu za kulitadarukia tatizo ambalo linakwamiza juhudi za maendeleo. Umaskini unaoyakabili mataifa yanayoendelea, unayatosa kwenye dhiki kubwa huku mataifa ya kimagharibi yakipiga hatua kubwa kimaendeleo. Ufa uliopo baina ya mataifa yanayoendelea na yale yaliyoendelea kama vile Marekani, nchi za Ulaya na Ujapani unapanuka kila uchao.

Vyanzo vya umasikini huu ni anuwai mathalan,ufisadi uongozi mbaya, turathi za kikoloni, uchumi kuegemezwa kwenye kilimo kinachotegemea mvua isiyotabirika, idadi ya watu inayoupiku uwezo wa uchumi wa taifa linalohusika na ukosefu wa nyenzo na amali za kuwakwamua raia kutoka lindi la umaskini. Ukosefu wa elimu na nafasi adimu za ajira huchangia pia katika tatizo hili.

Jamii ya ulimwengu inapaswa kuelewa kuwa umaskini, unaoathiri nchi fulani una athari pana sana. Uvunjifu natokana na umaskini unaweza kuwa mboji ambako matendo mabaya huchipuka. Raia maskini huweza kushawishiwa haraka kujitosa kwenye matendo ya kihalifu ili kujinasua kutoka dhiki ile. Hii inaweza kuwa mbegu ya kuatika maovu kama ugaidi na uhalifu wa kila aina.
Mataifa ya magharibi yanapaswa kuyaburia madeni mataifa yanayoendelea kama njia mojawapo ya kupambana na umaskini. Asilimia kubwa ya pato la kitaifa katika mataifa mengi hutumika kuyalipa madeni hayo. Katika hali hii inakuwa muhali kwa mataifa hayo kujikwamua kutokana na pingu za umasikini. Njia nyingine ni kustahabu kutoa ruzuku za kimaendeleo badala ya mikopo kwa nchi zinazoendelea.

Kwa upande wake, mataifa yanayoendelea yanapaswa kuibuka na mikakati bora ya kupambana na umaskini. Ni muhimu pawepo na sera zinazotambua ukweli kuwa asilimia kubwa ya raia wa mataifa hayo ni maskini. Pana dharura ya kuzalisha nafasi za ajira, kupanua viwanda hususan vinavyohusiana na zaraa ambayo ni tagemeo kuu la mataifa mengi, kuendeleza elimu na kuimarisha miundo msingi. Ipo haja pia ya mataifa haya kuhakikisha kuwa mfumo wa soko huru unaotawala ulimwengu sasa hauishii kuwa chanzo cha kufa kwa viwanda asilia na kuendeleza umaskini zaidi. Kwa ufupi, maamuzi yote ya sera za kiuchumi lazima yauzingatie uhalisi wa maisha ya raia wa mataifa hayo.

MASWALI

a) Kwa nini umaskini umetamalaki katika mataifa yanayoendelea? (alama 4)

……

……

……

……

……

b) Madeni yana athari gani kwa mataifa yanayoendelea? (alama 2)

……

……

……

c) Ni mapendekezo yapi ambayo mwandishi anatoa kwa mataifa machanga kuhusu utatuzi wa tatizo la umaskini? (alama 4)

……

……

……

……

……

d) Mfumo wa soko huru una madhara gani kwa mataifa machanga? (alama 2)

……

……

……

……

e) Ukirejelea kifungu, eleza maana ya:

(alama 3)

i) Kulitadarukia

……

……

ii) Kuatika

……

……

iii) Kuyaburia madeni

……

……

2. MUHTASARI

Ingawa baadhi yetu hufanya makosa tunapochagua marafki, ni vyema kuzingatia kwa makini sifa za rafiki yako. Kukosa kufanya hivi kunaweza kututia mashakani kwani rafiki mbaya anaweza kukuambukiza ubaya. Tusisahau kuwa **nazi mbovu harabu ya nzima**.

Kwa sababu hii, sifa nzuri ni nguzo ya urafiki: sifa nzuri hutufanya kufurahia pamoja bila hata wazazi wetu kuhofu chochote kwani urafiki huwa nipe nikupe.Hata hivyo, katika kusaidiana hatuwapi marafiki wetu mali au zawadi tu. Hii ni kwa sababu tunaweza hata kukosa pesa au zawadi za kuwapa marafiki ingawa tunawapenda. Kwa hivyo, katika urafiki tunabadilishana mawazo mbalimbali na kumwonyesha rafiki ni kwa nini tunampenda. Urafiki kama huu huwajenga wote wanaohusika.

Katika urafiki, ni vyema kuzingatia ukweli na uaminifu. Iwapo tunaishia kuwaiga marafiki au "kujifanya" ili kuwafurahisha marafiki kutupenda, basi, huenda tusifaidi kwa urafiki. Hii ni kwa sababu hali ya kuvalia ngozi ya kondoo kumbe tu simba mara nyingi huvunga urafiki baina ya watu pale sifa za mtu zinapojitokeza dhahiri kwani ukweli ukidhihiri uongo hujitenga. Hapo ndipo mmoja kati ya wale marafiki anapoanza kusema kuwa "afadhali ningejua." Hii ndio sababu watu huambiwa kuwa makini sana katika kuchagua marafiki na kuchukua muda kabla ya kuwaamini watu kuwa marafiki wetu wa dhati.

Pia, ili kufaidi katika urafiki ni vyema kuwa na rafiki ambaye umri wake na wako ni wa karibu. Rafiki kama huyu atakuwa huru kujadiliana nawe kuhusu yote yanayowahusu. Kwa upande mwingine, rafiki ambaye ana umri mkubwa zaidi ama mdogo sana kwako itakuwa shida kushirikiana naya kwa sababu mtazamo wake na wako kuhusu maswala mengi katika jamii utakuwa tofauti kabisa kama ardhi na mbingu. Hebu fikiri kuwa na rafiki ambaye huna uhuru kuzungumza naye yoyote utakayo kwa sababu unaomwogopa ama nafikiria yeye hataweza kukusaidi kimawazo.

Kuna hali nyingine ambayo tunapaswa kuepuka katika urafiki. Tunapofikiria kuhusu marafiki wanaotufaa, tunafaa kutozingatia mambo kama vile utajiri au pesa. Ikiwa tutazingatia swala kama hili katika kuwa na urafiki na mtu, basi, lazima tuwe tayari kwa kuharibika kwa urafiki huu wakati wowote. Hii ni kwa sababu urafiki

wenye misingi katika mambo kama hayo huisha wakati wowote mambo yanapokwenda mrama hasa kwa yule ambaye alikuwa akitegemea pesa hizi kwa urafiki. Pia, inaweza kuwa rafiki huyo hakupata pesa hizo kwa njia halali jambo ambalo linaweza kututia matatani. Lakini, hii haimaanishi tusiwe na marafiki ambao wanatoka katika jamii tajiri. Ikiwa urafiki wenu utakuwa na sifa zote zinazofaa bila hata kuzingatia mali yao, basi itakuwa sawa kabisa. Lazima tukumbuke kuwa urafiki ni tunu kubwa kwa maisha yetu hata bila pesa.

Kwa ujumla, ni muhimu kuzingatia kuwa urafiki hali kati ya wawili au zaidi anbayo inajengwa kwa muda na utaratibu. Huwezi kusema kuwa mtu ni rafiki baada ya muda mfupi kama hamjajuana kwa muda unaofaa. Ni lazima ichukue muda mjuane vizuri. Kukosana baina ya marafiki ndiko kujuana na kujenga urafiki wenye nguzo inayofa katika jamii.

Dondoa sifa kuu za kumchagua rafiki katika aya nne za mwanzo.

(maneno kati ya 30-40)

utiririko - (alama 6)

Matayarisho

……

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

a) Andika kwa ufupi yanayoangaziwa katika aya mbili za mwisho

(maneno kati ya 45-55)

matayarisho

……

……

……

……

……

Jibu

……

……

……

……

……

……

……

……

……

……

3. MATUMIZI YA LUGHA

a) (i) Taja sauti mbili ambazo ni irabu na wakati huo huo konsonanti. (alama 2)

……

……

(ii) Tambua sauti hafifu kati ya zifuatazo: (alama 1)

/K/, /r/, /gh/,/ sh/, /w/

……

……

b) Onyesha yambwa tendwa na yambwa tendewa katika sentensi hii. (alama 2)

Mbunge wa Mtondo Kaskazini atawajengea wanakijiji josho kisha aghurie mjini.

……

……

c) Andika kwa msemo taarifa (alama 3)

"Sitakwenda sokoni leo ila nitakwenda kesho," nikamjibu

……

……

d) Eleza matumizi ya neno wale katika sentensi hii.

Wale walioiba ni mabanati wale ambao waliambiwa wale kabla ya kitendo hicho.

……

……

……

e) Yakinisha sentensi hii. (alama 1)

Hapa napo sipo ninapotaka

……

……

f) Changanua kwa vielelezo vya mistari / vishale. (alama 3)

Mwanafunzi anapohepa shuleni huadhibiwa kikondoo.

g) Andika kwa udogo (alama 2)

Mtoto wa mzee yule aligongwa kwa nyundo alipofukuzwa na mbwa.

……

……

h) Tumia kiunganishi <u>alakulihali</u> katika sentensi ili kubainisha matumizi yake. (alama 1)

……

……

i) Akifisha sentensi hii

mtafanya kazi hii mpaka lini mzee alisema nataka ikamilike leo kesho mtaanza nyingine

……

……

j) Tunga sentensi ukitumia 'A'unganifu mwafaka pamoja na nomino ulizopewa (alama 2)

(i) Teo

……

……

(ii) Liwali

……

……

k) Eleza matumizi ya ni katika sentensi ifuatayo: (alama 2)

Rudini haraka! Amina **<u>ni</u>** mgeni hapa kwetu, nitamtembeza mjini

……

……

……

……

l) Vitumie vihisishi vifuatavyo katika sentensi. (alama 2)

(i) Ebo!

……

……

(ii) Kefule!

……

……

m) Sentensi hizi zinaashiria nyakati gani? (alama 2)

(i) Ninapokimbia huchoka sana

……

(ii) Aendapo msikitini hujitia tohara

……

n) (i) Imekuwa vigumu mwananchi kuelewa katiba

(andika katika kauli ya kutendea) (alama 1)

……

……

(ii) Andika sentensi katika kauli ya kutendewa ukitumia kitenzi 'cha'

(alama 1)

……

……

o) Tumia vivumishi vya pekee kutunga sentensi zenye maana ifuatayo. (alama 2)

(i) bila kubagua

……

……

(ii) bila kubakisha

……

……

p) Eleza maana mbili za sentensi hii (alama 2)

Alinichezea na Baniani

……

……

……

q) Tunga sentensi mbili tofauti kubainisha maana tofauti kati ya: (alama 2)

(i) Pamba

……

……

(ii) Bamba

……

……

r) Mwalimu huyu atawatahini wanafunzi wote watakaofanya mtihani. (alama1)

Anza: Wanafunzi wote

……

……

s) Unda kitenzi kutokana na nomino hii (alama 1)

Nomino ***kitenzi***

Ufisadi

4. ISIMU JAMII

Eleza huku ukitoa mifano mwafaka sifa tano za sajili ya bungeni. ` (alama 10)

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..

……..